

HAKI ZA WAKULIMA NA MKATABA WA MBEGU

Serikali za Afrika hazilindi haki za wakulima

Nchi 42 za Afrika zimeridhia **Mkataba wa Kimataifa kuhusu Rasilimali za Vinasaba vya Mimea kwa Chakula na Kilimo** (pia hujulikana kama 'Mkataba wa Mbegu'), ambao umeanza kutumika Juni, 2004.

Mkataba unatambua haki za wakulima kuhifadhi, kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu zilizohifadhiwa kutoka shamba na aina nyingine ya vipandikizi. Pia inalenga katika kulinda maarifa ya asili, kuzipa jamii haki ya kupata faida iwapo watu wengine watatumia maarifa yao au rasilimali kutengeneza bidhaa za biashara. Mkataba wa Mbegu unaziamuru serikali kufanya yafuatayo:

- ◆ kuhakikisha kwamba wakulima wanashiriki katika kufanya maamuzi kuhusu masuala yanayohusiana na mbegu na vipandikizi; na
- ◆ kutekeleza haki za wakulima kurudia kutumia na kubadilishana mbegu zilizohifadhiwa kutoka shamba.

Kwa bahati mbaya, serikali za Afrika hazijatekeleza wajibu wowote katika hayo.



Sheria ya Afrika ya Mfano

Katika ngazi ya bara, kuna **Sheria ya Afrika ya Mfano kuhusu Ulinzi wa Haki za Jamii za Wenyeji, Wakulima na Wazalishaji wa Mbegu, na Udhhibiti wa Upatikanaji wa Rasilimali za Kibaiolojia**. Sheria hii inatambua na kusawazisha aina mbalimbali za haki, pamoja na:

- ◆ haki za wazalishaji wa mimea;
- ◆ haki za wakulima kama wazalishaji wa mbegu; na

- ◆ haki za wakulima kurudia kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu zote zilizohifadhiwa kutoka shamba (Haki za Wakulima).

Sheria ya Afrika ya Mfano hairuhusu hakimiliki (umiliki) kwenye viumbe hai kama vile mbegu na vipandikizi.

Hata hivyo, sheria hii pia imepuuzwa na serikali za Afrika.

